# TAARIFA YA VIWANDA HALMASHAURI YA WILAYA NGARA

## UTANGULIZI

Tunapozungumzia viwanda, kuna maana tofauti tofauti zinazoelezea viwanda. Lakini kwa hivi sasa tunamaanisha kuwa viwanda ni Mfumo uliotengenezwa kwa lengo la kuandaa, kutengeneza na kutoa bidhaa zinazohitajika kwa mahitaji mbali mbali ya binadamu na au kwa ajili ya viwanda vingine, nje ya mfumo wa kilimo au ufugaji.

Aidha, kwa mjibu wa sera ya SIDO ya mwaka 2002 viwanda vimegawanyika katika makundi makuu manne, yaani viwanda vidogo sana, vidogo, vya kati na vikubwa. Mchanganua na vigezo vyake ni kama jedwali linavyoonesha hapo chini;

## MIKAKATI YA MASUALA YA VIWANDA

Katika kipindi cha miezi sita (6) Ofisi ya Mkurugenzi imejiwekea mikakati ya kutekeleza shughuli zifuatazo; kufanya utambuzi wa viwanda vilivyopo wilayani, kufanya vikao vya uhamasishaji na wadau wa viwanda, kuratibu maandalizi ya maeneo (Site) kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda, kuandaa semina na mafunzo kwa ajili ya kuhamasisha uwekezaji wa ndani kwenye viwanda, kuandaa mkakati maalum kwa ajili ya viwanda vidogo sana, vidogo na vya kati.

## UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO YA VIWANDA

| NA. | **Aina ya kiwanda** | **Waajiriwa kwenye Kiwanda** | **Mtaji wa Kiwanda katika (Tshs.)** |
|---|---|---|---|
| 01 | Viwanda Vidogo Sana | 1 – 4 | Hadi Mill. 5. |
| 02 | Viwanda Vidogo vya Kati | 5 – 49 | Juu ya Mill 5. Hadi Mill. |
| 03 | Viwanda vya Kati | 50 – 99 | Juu ya Mill. 200 Hadi Mill.800. |
| 04 | Viwanda Vikubwa. | 100 + | Juu ya Mill. 800. |

Katika kutekeleza azma ya Uchumi wa viwanda yafuatayo yamefanyika,

- Kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda na hasa vikubwa na vya kati kwa ngazi ya Halmashauri kumetengwa eneo katika kijiji cha Lwakaremela kata ya Kasulo.
- Maelekezo yalishatolewa kila kijiji kutenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda kwa hivi sasa zoezi la kuhakiki maeneo hayo linaendelea.
- Tarehe 06/02/2018 kiliitishwa kikao cha wawakilishi wa wafanyabiashara na wadau wengine kwa ajili ya kuzungumzia masuala yanayohusu uwekezaji wa viwanda ambapo yafuatayo yalizungumziwa; Maelezo kuhusu malengo ya viwanda kwa ufupi, maana na aina za viwanda, fursa zilizopo wilayani kwa ajili ya ujenzi wa viwanda, maelekezo ya serikali kuhusu ujenzi wa viwanda, mapendekezo ya viwanda na maeneo ya kujenga viwanda, namna ya upatikanaji mitaji mikubwa kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda kwa ushirikiano kati ya halmashauri na wadau wengine (ppp), maoni na maazimio.
- Zoezi la uhakiki viwanda ili kuwezesha ufaham wa ni viwanda vingapi vilivyopo na vya aina gani linaendelea kwa kuanzia kata ya Ngara Mjini. Aidha, kwa

uhakiki uliokwishafanyika hapa Ngara Mjini, viwanda 32 vimehakikiwa, ambavyo vimewaajiri wakazi 155, na vimewekeza mitaji ya Shilingi 386,360,000/=. Kati ya viwanda hivyo 12 ni vidogo sana, na 20 ni vidogo. Taarifa ya uhakiki kwa hatua iliyofikiwa imeambatanishwa.

**CHANGAMOTO**

Aidha, katika shughuli za viwanda zipo changamoto zilizojitokeza kama vile;

- Wanajamii walio wengi, hawaelewi nini hasa maana ya viwanda, na tunapozungumza viwanda tunamaanisha ni vya aina gani na kwa malengo gani
- Katika maeneo mengi ya wilaya tunavyo viwanda, lakini hatutambui na kwa kuwa hatuvifahamu hatutambui ni vingapi na vya aina gani na hata maeneo yaliyotengwa haifahamiki ni ya akina nani.
- Lipo tatizo la uvamizi wa maeneo yanayotengwa kwa ajili ya viwanda, na hata baadhi ya wahusika muhimu, kuyasahau maeneo hayo. Mf. Eneo linalofahamika na wanajamii kuwa la viwanda lililoko kati ya Ujenzi (Gereji ya Halmashauri) na Samma Gereji.
- Watu wetu hawana bidii na ufahamu wa kuwawezesha kuwekeza katika viwanda vya kati na vikubwa.
- Kazi ya kuhakiki viwanda hivi ni ngumu kutokana na ugumu wa wahusika kutoa taarifa zinazotakiwa, hivyo zoezi litachukua siku zaidi ya ilivyotarajiwa.
- Uhaba wa Rasilimali fedha kwa ajili ya wakati wa utekelezaji shughuli za viwanda

**USHAURI NA MAPENDEKEZO YA UTATUZI WA CHANGAMOTO**

Pamoja na shughuli zingine yafuatayo ni muhimu yakafanyika kuhakikisha baadhi ya changamoto zinatatuliwa;

- Kutolewe Elimu ya masuala ya ujasiliamali kwa wenye viwanda vidogo sana na vidogo.
- Maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya viwanda yalindwe kwa nguvu zote yasivamiwe na kwa maeneo yaliyovamiwa wavamizi waondolewe.
- Zoezi la uhamasishaji na uhakiki wa viwanda vilivyopo pamoja na uwekezaji wa viwanda kwa ujumla upewe kipaumbele zaidi na kuwezeshwa rasilimali fedha, na wadau mbalimbali watakao takiwa kuwezesha.

Imeandaliwa na;

SYPRIANI G. MUHERANYI

**MRATIBU WA MAENDELEO YA VIWANDA**

**Kny. MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA WILAYA**